## Maswali

1. Waisraeli walipigani na nani?
2. Waisraeli wangapi waliuawa mara ya kwanza?
3. Waisraeli walileta nini ili iwasaidia kwa vita?
4. Nini ilifanyika kwa vita siku ifuatayo?
5. Mbona Sanduku halikuwasaidia Waisraeli?
6. Nini ilifanyika kwa Eli baada ya kusikia habari ya Sanduku?
7. Wafilisti walipeleka Sanduku wapi?
8. Nini ilifanyika kwa Dagoni sanamu yao?
9. Nini ilifanyika kwa Wafilisti Sanduku ilipopelekwa kwa miji yao?
10. Wafilisti walipelekea Waisraeli Sanduku namna gani?

## Majibu

1. Waisraeli walipigana na Wafilisti.
2. Waisraeli 4,000 waliuawa mara ya kwanza.
3. Waisraeli walileta Sanduku kutoka Shilo.
4. Waisraeli 30,000 waliuawa. Wana wawili wa Eli walikufa. Sanduku lilichukuliwa na Wafilisti.
5. Watu hawakuamini Mungu, kwa hivyo Sanduku halingewasaidia.
6. Eli alianguka kutoka kwa kiti, akavunjika shingo na akafa.
7. Wafilisti walipeleka Sanduku kwa mji wa Ashdodi.
8. Sanamu Dagoni ilianguka kwa sakafu. Halafu kichwa na mikono yake zilikatika.
9. Wafilisti walikuwa wagonjwa kutokana na tauni na wengi walikufa.
10. Waliweka Sanduku na zawadi juu ya gari mpya lililofutwa na ng'ombe wa ndama. Ng'ombe waliacha ndama na kuenda mpaka nchi ya Israeli.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 2

# 56 Wafilisti wanatwaa Sanduku

### Kwa Biblia

1 Samweli milango ya 4, 5, 6 na 7

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni la maana kuamini Mungu. Mungu ni Mungu wa kweli. Hakuna miungu mingine

### Somo

Samweli alipokua alikuwa nabii mwaminifu wa Mungu. Waisraeli wengi walikuwa wamesahau Mungu. Waliabudu sanamu. Samweli alijaribu kuwafundisha juu ya Mungu.

Wafilisti waliendelea wakishambulia Waisraeli. Waliiba mazao yao. Waisraeli wakawa maskini na hawakuwa na chakula cha kuwatosha.

Waisraeli waliaamua kupigana na Wafilisti. Waisraeli hawakukuwa na silaha nzuri.Hawakukuwa na nguvu kama Wafilisti. Waisraeli hawakuamini kwa Mungu ili awasaidie. Siku ya kwanza ya vita, Wafilisti waliua Waisraeli 4,000

Waisraeli waliogopa. Wangeshinda namna gani vita tena. Mmoja wao akakumbuka kwamba miaka mingi iliyopita Waisraeli walienda na Sanduku la Mungu vitani. Hapo walikuwa wakishinda vita.

Sanduku la Mungu liliwekwa katika nyumba ya Mungu huko Shilo. Wajumbe walikimbia kwenda kuleta. Wana wawili wa Eli walibeba Sanduku wakapeleka kwa kambi ya Waisraeli. Waisraeli walipiga shangwe na vikelekele kuu walipoona Sanduku. Wafilisti walikuwa na uoga. Walijua kwamba Waisraeli walikuwa wakishinda vita wakati Sanduku la Mungu lilikuwa nao.

Waisraeli walifikiri watashinda vita siku hiyo. Walikuwa wana Sanduku la Mungu. Lakini hawakushinda vita. Wafilisti waliua Waisraeli 30,000. Wana wawili wa Eli waliuawa. Sanduku lilitwaliwa na Wafilisti.

Mjumbe alikimbia Shilo akipeleka habari mbaya. Watu wote wa Shilo waliomboleza waliposikia habari. Eli aliposikia kwamba Sanduku limetwaliwa, alianguka nyuma kutoka kwa kiti alichokalia. Eli alipoanguka alivunjika shingo na akafa. Unabii ulionenwa na Mungu kwa Samweli ulitimizwa.

Lakini mbona Sanduku halikuokoa Waisraeli? Sanduku lilikuwa limeokoa Waisraeli huko nyuma kwa sababu ilikuwa ishara kwamba Mungu alikuwa nao. Wakati wa Samweli, Waisraeli hawakupenda Mungu. Hawakuomba Mungu na kutaka usaidizi wake. Hawakuamini Mungu. Walichukuwa Sanduku kutumia kama hirizi ya baraka au bahati. Kwa hivyo Mungu hakukuwa nao.


*Dagoni*

Wafilisti walibeba Sanduku kwa shangwe wakipeleka Ashdodi. Waliweka Sanduku ndani ya hekalu ya sanamu yao—Dagoni. Asubuhi yake walipata hiyo sanamu Dagoni imelala chini kifudifudi mbele ya Sanduku. Wafilisti walirudisha Dagoni pahali pake. Asubuhi ingine tena, sanamu Dagoni ilikuwa imeanguka chini. Kichwa na mikono yake zilikuwa zimekatika.

Mungu alituma tauni kwa watu wa Ashdodi. Waligonjwa sana, hata wengi wao walikufa. Watu wa Ashdodi waliogopa. Walichukua Sanduku wakalipeleka kwa mji wa Gathi.

Bunde tu Sanduku lilipofika huko Gathi, watu walianza kuwa wagonjwa na wengi wakafa. Watu wa Gathi walipeleka Sanduku kwa mji wa Ekroni. Watu wa Ekroni nao waliogopa . Walijua kilichofanyika kwa watu wa Ashdodi na Gathi.

Sanduku lilipowasili Ekroni, watu walianza kufa kutokana na tauni. Watu wa Ekroni waliuliza watu wao wa hekima ni nini watafanya hilo Sanduku.

Watu wao wa hekima waliwambia watengeneze gari mpya . Wafunge ng'ombe wa kike wawili wenye wana ndama wadogo. Lazima waweke Sanduku kwa hilo gari. Lazima tena waweke dhahabu kama zawadi juu ya hilo gari. Watu wa hekima waliwambia wafunge ndama na waachilie ng'ombe waende na gari. Ikiwa hawa ng'ombe wawili watarudi kutafuta ndama wao inamaanisha ilikuwa kawaida tauni kuwa kwa miji ya Wafilisti. Lakini ikiwa ng'ombe wataendelea na safari ya kurudishia Waisraeli Sanduku, itamaanisha ni Mungu alikuwa ametuma tauni. Tena watu wa hekima wakawambia kwamba Mungu atawasamehe wakipeleka Sanduku pamoja na zawadi.

Watu wa Ekroni walitengeneza gari mpya. Walichukua ng'ombe wawili waliokuwa na ndama. Walifunga wale ng'ombe wawili kwa gari. Waliweka Sanduku na dhahabu juu ya gari. Mwishowe walifungia ndama nyumbani na kuwaachilia ng'ombe waende.

Ng'ombe hawakurudi kwa ndama wao. Ng'ombe walienda wima barabarani mpaka kwa nchi ya Israeli.

Kijiji cha Beth-shemeshi kiko kwa mipaka ya Israeli. Watu wa Beth-shemeshi walikuwa shambani. Walikuwa wanavuna ngano yao. Waisraeli walishangaa kuona gari linarudisha Sanduku la Mungu. Waisraeli walitolea Mungu sadaka ya shukrani kwa kuwarudishia Sanduku. Sanduku lilipelekwa Kiriath Yearimu. Sanduku liliwekwa kwa nyumba huko Kiriath Yearimu kwa miaka ishirini.

